JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L.P 30261
Simu: (023) 2402658
Nukushi: (023) 2402657
Barua pepe: rbcpwani@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

PWANI-APRIL 21, 2020

TAKUKURU MKOA WA PWANI YAZIDI KUIMARISHA NGUZO ZA UTAWALA BORA KWA KUDHIBITI RUSHWA KATIKA MIRADI YA MAENDELEO NA KUOKOA TSHS. 168,405,130.87 KUPITIA UCHUNGUZI

Ndugu waandishi wa habari,

Ni utaratibu wa TAKUKURU kutoa taarifa ya utendaji kazi kwa kila robo ya mwaka ili kuujulisha umma juu ya kazi zilizofanyika ili kuhamasisha umma kuongeza imani na kushiriki mapambano dhidi ya rushwa.

TAKUKURU mkoa wa PWANI imefanya mambo yafuatayo katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Machi, 2020

UCHUNGUZI NA MASHITAKA

Katika kipindi hiki ofisi ilifanya operesheni mbalimbali za uchunguzi mkoani na wilayani ambapo jumla ya kiasi cha **shilingi milioni Mia moja sitini na nane laki nne na elfu tano mia moja na thelathini na senti themanini na saba (168,405,130.87)** ziliokolewa kupitia operesheni hizo. Fedha hizo zinatokana na:

- Kiasi cha **shs. 4,000,000/-** ni faini kwa wafanyabiashara wa mazao ya misitu ambao walikiuka taratibu za uvunaji wa mazao ya misitu wilayani Rufiji.

- Uchunguzi wa mapato kupitia machimbo ya mchanga huko Bagamoyo ambapo jumla ya **shs. 29,000,000/-** zilirejeshwa serikalini kutoka kwa wafanyabiashara na wakusanyaji mapato waliosababisha upotevu wa fedha hizi.

- Kiasi cha **shs. 16,217,770/-** kiliokolewa kutoka kwa watumishi waliopewa dhamana ya kukusanya mapato kupitia mashine za mauzo (POS) kwa wilaya za Rufiji na Kibiti.

- Kiasi cha Shs **15,500,000/-** ziliokolewa baada ya kulipwa kinyume na taratibu katika ujenzi wa hospitali ya wilaya ya Kibiti ambapo mzabuni alilipwa malipo hewa ya vifaa kwani mzabuni alilipwa fedha za kuwasilisha vifaa lakini uchunguzi ulibaini kuwa vifaa hivyo havikuwasilishwa.

- Ofisi ya TAKUKURU wilaya ya Rufiji ilifanikiwa kurejesha **shs. 1,176,000/-** zilizotokana na kuibwa kwa bati 33 kati ya bati 166 zilizonunuliwa kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya wanaume katika hospitali ya wilaya ya Rufiji. Fedha hizo zimerejeshwa katika akaunti ya hospitali ya wilaya ili zikafanye shughuli nyingine za umma.

- Kiasi cha **shs. 5,000,000/-** kilipatikana kutoka kwa mfanyabiashara wa chuma chakavu aliyekiuka sheria za mazingira kwa kusafirisha malighafi ya chuma chakavu pasipokuwa na leseni ya ukusanyaji na usafirishaji.

- Kiasi cha **shs. 210,000/-** ambacho kilikuwa ni mshahara wa walinzi watatu wa Soko la kijiji cha Umwe huko Ikwiriri kilichokuwa kimechepuchwa, kilirejeshwa kwa wahusika baada ya TAKUKURU kufuatilia na walinzi hao kulipwa pesa zao.

- Kiasi cha **shs. 5,000,000/-** kiliokolewa kutoka kwenye mradi wa ujenzi wa barabara KN 52 ya wilayani Mafia ambapo mkandarasi hakufanya vipimo vya ubora wa vifaa (Nondo), mradi huo ulikataliwa na Kiongozi wa mbio za mwenge wa uhuru mwaka 2019.

- Kiasi cha **shs. 91,218,360.87** ni urejeshwaji wa fedha za korosho na zao la ufuta kwa wananchi ikiwa ni mwendelezo wa ufuatiliaji wa ofisi yangu kwa agizo la Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI na mtakumbuka robo iliyopita ofisi yangu ilirejesha kiasi cha **shs. 217,481,498/-**

Aidha, jumla ya **kesi 26** ziliendelea kuendeshwa katika mahakama mbalimbali za mkoa wa Pwani ambapo **kesi 4** zilitolewa hukumu. Katika kesi hizi upande wa Jamhuri ulishinda kesi hizo zote kwa washitakiwa kuamuliwa kufungwa jela au kulipa faini ambapo watuhumiwa wawili walilipa faini mmoja alilipa shilingi 1,000,000/- na mwingine alilipa shilingi 300,000/- na mwingine alienda kutumikia kifungo cha miaka minne jela na wa mwisho ambaye alikuwa Afisa Ardhi msaidizi wilaya ya Mafia alifungwa miaka saba jela.

Pia tuliwafikisha mahakamani Afisa Mipango pamoja na Afisa Ardhi wa Halmashauri ya mji wa Chalinze kwa kuomba na kupokea Rushwa ya shs. 127,000,000/-. Hayo ni matunda ya jamii kuielewa TAKUKURU na kutoa ushirikiano katika mapambano hususani katika utoaji wa taarifa na ushahidi mahakamani.

Ofisi ilipokea malalamiko **153** kati ya hayo malalamiko **88** uchunguzi wake unaendelea katika hatua mbalimbali na malalamiko **65** yalionekana kuangukia katika sheria nyinginezo hivyo walalamikaji walishauriwa na kuelekezwa sehemu husika kwa lengo la kutatua kero zao.

ELIMU KWA UMMA.

Ndugu waandishi wa habari,

Kwa kipindi hicho ofisi imeendelea kutoa elimu kwa jamii kwa njia mbalimbali za uelimishaji ambapo semina **106** zimetolewa, mikutano **57** imefanyika, klabu za wapinga rushwa 21 zimefunguliwa na **49** zimeimarishwa, maonesho **7** yamefanyika na vipindi **2** vya redio vilifanyika.

Aidha kwa njia ya vipindi vya Redio mubashara ofisi ilitoa elimu ya juu ya UMUHIMU WA KUSIMAMIA MIRADI YA MAENDELEO ambapo umma wa watanzania umehamasika sana kupitia vipindi hivyo na kuunga mkono vita dhidi ya Rushwa bila woga, pia kupitia vipindi hivi ilitolewa elimu juu ya Kampeni ya VUNJA UKIMYA KATAA RUSHWA YA NGONO, hii ni rushwa inayoharibu na kushusha utu wa mwanadamu na kuleta madhara makubwa kiuchumi - kwani sote tumeshuhudia sasa ongezeko la wanaoathirika na rushwa hii kufika TAKUKURU na kutoa taarifa za kuombwa ama kulazimishwa rushwa za ngono. Hayo yote ni matunda ya kampeni hii kupitia vipindi vya redio kinyume na awali.

Kupitia klabu za wapinga rushwa TAKUKURU imeendelea kutoa elimu juu ya madhara ya Rushwa kwa jamii na kuhamasisha vijana kuwa wazalendo kwa nchi yao kukemea vitendo vya Rushwa nchini. Kwani waswahili wanasema samaki mkunje angali mbichi. Ni imani ya TAKUKURU kuwa vijana hawa watakuwa viongozi bora na waadilifu hapo baadae kwa kupinga rushwa kwa vitendo.

UZUIAJI RUSHWA

Katika eneo la Uzuiaji Rushwa tulifanya uchambuzi wa mifumo 13 katika maeneo mawili ambayo ni; mfumo wa usimamizi na uendeshaji wa vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS) na ufuatiliaji wa uchambuzi wa mfumo wa miundombinu ya barabara zinazosimamiwa na Mamlaka ya Barabara Vijijini (TARURA). Malengo ya kufanya uchambuzi wa mifumoni kubaini mianya ya rushwa na kutafuta mbinu za kuziba mianya hiyo.

Baadhi ya mianya iliyobainika katika ufuatiliaji wa usimamizi wa vyama vya msingi ni pamoja na vyama vingi kutokuwa na wataalam wa masuala ya fedha hivyo wajumbe/wanachama miongoni mwao ndio wanatumika kama wahasibu. Hii ni changamoto kwa kuwa wengi wao hawatunzi kumbukumbu za mahesabu na kusababisha upotevu wa fedha ama ubadhirifu, pia maafisa ushirika kutotembelea mara kwa mara AMCOS zao kuona kama zinajiendesha kwa mujibu wa sheria na hivyo kupelekea bodi au uongozi wa AMCOS kuendesha ushirika kwa mazoea bila kufuata taratibu, na viongozi wengi wa AMCOS hupatikana kwa njia za Rushwa wakati wa uchaguzi.

UFUATILIAJI WA MIRADI

Ndugu waandishi wa habari,

Mtakumbuka kuwa ni jukumu la TAKUKURU kuhakikisha kuwa miradi ya maendeleo katika nchi yetu inakuwa na tija na kuleta matunda yaliyokusudiwa. Katika robo hii ya mwaka tumekagua jumla ya miradi ya maendeleo 15 katika sekta za elimu, ujenzi, maji, barabara na Afya. Miradi hiyo ina thamani ya shilingi **Bilioni tisa na milioni mia nne hamsini na tatu laki mbili na elfu ishirini mia saba tisini na saba na senti ishirini na nane (shs. 9,453,220,797.28)**.

Aidha katika ufuatiliaji wa miradi hiyo baadhi ya miradi ilibainika kuwa na mapungufu yaliyotokana na ukiukwaji wa taratibu za manunuzi ya umma, na baadhi ya wazabuni kulipwa malipo bila kukata kodi ya serikali (Withholding Tax) na hivyo kuikosesha mapato serikali. Wakurugenzi wa Halmashauri husika wameelekezwa kukata fedha hizo na kuahidi kuchukua hatua.

Pia baadhi ya miradi ilikuwa na mapungufu kama vile majengo kupauliwa kwa mabati ya gauge 30 badala ya gauge 28 kinyume na mkataba. Kwa mfano katika mradi wa ujenzi wa madarasa matatu ya shule ya msingi NYAMBANGALA wilayani Kibiti mkandarasi alipauwa madarasa hayo kwa bati za gauge 30 kinyume na mkataba uliomtaka kupauwa kwa bati za gauge 28. Mapungufu hayo yamefanyiwa kazi kwa mkandarasi kaelekezwa kupitia kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya ya Kibiti kupauwa upya kwa bati za gauge 28.

Katika mradi wa ujenzi wa hospitali ya wilaya ya Kibiti mkataba ulimtaka mkandarasi kuweka milango ya mbao za mkongo lakini **kati ya milango 126 ni milango 13 tu ilikuwa ya mbao za mkongo, milango mingine 113 ilikuwa ya mbao mchanganyiko** hivyo kukosa ubora uliotakiwa. Mkurugenzi ameelekezwa kumtaka mkandarasi huyo kuondoa milango hiyo na kuweka milango inayotakiwa.

MIKAKATI YETU KWA KIPINDI CHA APRILI MPAKA JUNI 2020

Kama ilivyo dira ya Taifa kuelekea uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani mwaka huu, mikakati ya mkoa wa Pwani ni kuhakikisha uchaguzi huu unafanyika pasipo kuhusisha vitendo vya Rushwa kwa kufanya yafuatayo;

- Kufikisha elimu ya madhara ya Rushwa kwa wananchi wote mpaka ngazi ya kijiji ili waone umuhimu wa kuchagua viongozi waadilifu watakaokuwa mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi wakati wa uchaguzi.

- Kuendeleza mapambano dhidi ya Rushwa kwa kutumia mbinu za kisasa zaidi kwani tayari wachunguzi wa mkoa huu wamepata mafunzo ya kitaalam ya kuchunguza Rushwa kubwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa, hii itasaidia zaidi kuchunguza makosa kama vile uhujumu uchumi, utakatishaji wa fedha na limbikizo la mali.

WITO WA TAKUKURU KWA WANANCHI

Ndugu waandishi na wananchi,

Naomba kutumia fursa hii kuwasihi wananchi wa mkoa wa Pwani na watanzania kwa ujumla kuwa wazalendo kwa nchi yao kwa kuwafichua watakaojihusisha na vitendo vya Rushwa katika uchaguzi ujao kwa kutoa taarifa TAKUKURU kupitia namba za BURE 113 AU kwa ujumbe mfupi wa simu kwa kupiga *113# kisha fuata maelekezo kwani kuna baadhi ya watumishi wa serikali wameshaanza kutumia muda wa mwajiri wao kujitangaza na kuonyesha nia na wengine kufanya vitendo visivyokuwa vya kiungwana dhidi ya wenzao walioonyesha nia.

Aidha kuna wimbi la MATAPELI wanaojifanya ni watumishi wa idara za serikali yaani maafisa Usalama wa Taifa ama maafisa wachunguzi wa TAKUKURU. Natoa wito kwa wananchi kupitia ninyi waandishi, pindi unapopigiwa simu na kuitwa na mtu yeyote aliyejitambulisha ni afisa wa TAKUKURU tafadhali fika katika ofisi za TAKUKURU zilizopo jirani ili kujiridhisha na wito huo. Watu wengi wametapeliwa kupitia utaratibu huu. Hivyo ninawasihi wananchi kutoa ushirikiano kwa ofisi hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mujibu wa sheria.

Asanteni kwa kunisikiliza!

Imetolewa na:

Suzana Raymond

MKUU WA TAKUKURU (M)
PWANI